**SOMO: JINSI YA KUWA MKRISTO KATIKA MAZINGIRA YA KISIASA**

1 **Petro 2:13–17**

1 Petro 2
13 Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana; ikiwa ni mfalme, kama mwenye cheo kikubwa;
14 ikiwa ni wakubwa, kama wanaotumwa naye ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya na kuwasifu watenda mema.
15 Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu;
16 kama walio huru, ila wasioutumia uhuru huo kwa kusitiri ubaya, bali kama watumwa wa Mungu.
17 Waheshimuni watu wote. Wapendeni ndugu. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme.

UTANGULIZI

Kila baada ya miaka mitano, taifa letu la Tanzania linaingia katika kipindi cha uchaguzi mkuu. Ni wakati ambao mara nyingi watu hujawa na hisia kali, maneno makali, na mivutano ya kisiasa. Wapo wanaosema, “Kama fulani hatashinda, nchi imekwisha,” au “Kama huyu atashinda, hatuna tumaini tena.”
Lakini swali ni hili:
Mkristo anapaswa kujiendesha vipi katika wakati kama huu?
Tunapaswa kutambua kwamba sisi siyo tu raia wa Tanzania bali ni raia wa Ufalme wa Mungu.

1. TIINI KILA MAMLAKA KWA AJILI YA BWANA (1 Petro 2:13–15)

Neno “tiini” linamaanisha kukubali mamlaka na kuheshimu uongozi uliopo.
Petro aliandika maneno haya wakati Nero akiwa mfalme wa Roma mtu katili na asiye mwema.
Hata hivyo, Mungu kupitia Petro alisema:

“Tiini kila mamlaka ya kibinadamu kwa ajili ya Bwana...”

Hii ina maana kuwa tunapoheshimu viongozi, tunamtii Mungu.
Tunapokataa, tunampinga Mungu aliyewaweka.

Warumi 13:1–2 inasema:

“Kila mtu na atiini mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyoko imewekwa na Mungu. Hivyo anayeipinga mamlaka, anapinga agizo la Mungu.”

Hata kama hatupendezwi na mgombea fulani, tunapaswa kutenda mema na kuonyesha tabia njema, ili — kama Petro anavyosema “tunyamazishe ujinga wa watu wasiojua.”

Wakristo hawapaswi kushiriki katika matusi, majigambo, au chuki za kisiasa.
Tunapaswa kuonyesha upendo, heshima, na hekima.
Kura yetu ni wajibu wa kiraia; tabia yetu ni ushuhuda wa kiroho.

2. ISHI KAMA WATUMWA WA MUNGU (1 Petro 2:16)

Petro anasema:

“Kama watu huru, lakini msiutumie uhuru wenu kuwa kisingizio cha uovu, bali kama watumwa wa Mungu.”

Tanzania ni nchi huru. Tuna uhuru wa kusema, kufikiri, na kupiga kura.
Lakini Mkristo hatumii uhuru wake kuharibu amani, kuchochea ghasia, au kusema maneno ya chuki.
Uhuru wetu unapaswa kuonyesha kwamba sisi ni watumwa wa Mungu, si wa matamanio au mihemko ya kisiasa.

Yesu mwenyewe alitupa mfano katika Mathayo 17:24–27 alipolipa kodi.
Ingawa alikuwa Mwana wa Mungu — na hakuwa chini ya mamlaka ya kifalme ya kibinadamu — alisema:

“Lakini tusije tukawakwaza, nenda baharini ukavue samaki, katika kinywa chake utapata shekeli, ichukue ukalipie mimi na wewe.”

Yesu aliheshimu mamlaka ya dunia ili asilete kikwazo kwa watu.
Hivyo nasi, katika uchaguzi huu, hatupaswi kuwa kikwazo kwa watu kumjua Kristo kwa sababu ya maneno au matendo yetu ya kisiasa.

3. MAAGIZO MANNE KWA MKRISTO (1 Petro 2:17)

(1) Waheshimuni Wote

Usimdhihaki mtu kwa sababu ya chama chake, kabila, au maoni yake ya kisiasa.
Kila mtu ameumbwa kwa mfano wa Mungu.
Heshima ni ushuhuda wa upendo wa Kristo ulio ndani yetu.

(2) Wapendeni Ndugu

Kumbuka, kabla hatujaitwa Wapinzani au Wafuasi, tumeitwa Wakristo.
Usiache siasa ziharibu upendo wa kindugu kanisani.
Udugu wetu wa kiroho ni wa kudumu kuliko siasa za muda.

(3) Mcheni Mungu

Kabla ya kusema, kupost, au kupiga kura, uliza:
“Je, jambo hili linamcha Mungu?”
Hofu ya Mungu ndiyo itakayotuongoza kufanya yaliyo sahihi, siyo hisia za kisiasa.

(4) Mheshimuni Mfalme

Katika lugha yetu ya leo — Mheshimuni Rais, viongozi, na mamlaka zilizopo.
Heshima hii si kwa sababu wao ni wakamilifu, bali kwa sababu Mungu ndiye aliyewaweka.
Tunawaheshimu kwa ajili ya Bwana, tukijua kwamba Mungu ndiye anayeinua na kuangusha viongozi.

HITIMISHO

Uchaguzi ukifika tarehe 29 Oktoba, na matokeo yakitangazwa,
iwe mgombea wako ameshinda au ameshindwa,
kumbuka haya:

Tiini kila mamlaka kwa ajili ya Bwana.

Tenda mema ili kunyamazisha ujinga wa wasiojua.

Ishi kama mtumwa wa Mungu.

Waheshimu wote, mpeni upendo ndugu, mcheni Mungu, mheshimu kiongozi.

Tujue kwamba sisi ni raia wa mbinguni, na Yesu Kristo ndiye Mfalme wetu wa milele.
Tanzania ni nchi yetu ya muda, lakini Ufalme wa Mungu ni wa milele.
“Tuishi kama nuru katikati ya giza hili la kisiasa,
tuseme kama Wakristo,
tupige kura kama Wakristo,
na baada ya uchaguzi tuendelee kuishi kama Wakristo.”